**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAJI**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

"Maji Bombani"

# WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI



# TAARIFA YA UTENDAJI WA RUWASA KWA MWAKA 2020/2021

**MEI, 2022**



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) (mwenye mkasi) akizindua mradi wa maji.

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency
"Maji Bombani"

# Huduma ya maji safi na salama, ya kutosha na ya uhakika pamoja na huduma ya usafi wa mazingira.

Chapisho hili limeandaliwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na OIKOS kwa ufadhili wa kifedha kutoka Italian Agency for Development Cooperation (AICS).

OIKOS

ITALIAN AGENCY FOR DEVELOPMENT COOPERATION

Imesanifiwa **MediaOne** Multimedia

# YALIYOMO

BARUA YA KUWASILISHA TAARIFA ..... ii
UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI ..... iii
UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU ..... v
VIFUPISHO VYA MANENO ..... vii
1. UTANGULIZI ..... 1
1.1 Uanzishwaji wa RUWASA ..... 1
1.2 Dira, Dhima, Tunu ..... 1
1.3 Muundo wa Utendaji na Utawala ..... 2
2. VYANZO VYA FEDHA VYA RUWASA ..... 5
2.1 Vyanzo Vya Ndani ..... 5
2.2 Vyanzo Vya Nje ..... 5
3. MALENGO NA MIPANGO ..... 6
4. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA RUWASA KATIKA MWAKA 2019/20 ..... 6
4.1 Bajeti ya Kufanikisha Mipango kwa 2019/2020 ..... 7
4.2 Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mipango ..... 7
4.2.1 Fedha Zilizopokelewa Kwa Mwaka 2019/2020 ..... 7
4.2.2 Kazi Zilizotekelezwa Kwa Mwaka 2019/2020 ..... 9
5. SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2020/2021 ..... 10
5.2 Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mipango ..... 11
5.2.1 Fedha Zilizopokelewa ..... 11
5.1 Bajeti ya Kufanikisha Mipango ..... 11
5.2.2.1 Uboreshaji wa Utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini ..... 13
5.2.2 Kazi Zilizotekelezwa ..... 13
5.2.2.2 Utoaji wa Huduma Endelevu ya Maji ..... 15
5.2.2.3 Uanzishwaji na Uimarishaji wa RUWASA ..... 15
5.2.2.4 Uboreshaji wa Huduma ya Usafi wa Mazingira Vijijini ..... 16
5.2.2.5 Uboreshaji wa Utendaji wa Rasilimaliwatu ..... 17
5.2.2.6 Uimairishaji wa Uwezo na Usimamizi wa Kifedha ..... 19
5.2.2.7 Kujenga Taswira ya Taasisi ..... 20
6. MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI ..... 20
6.1 Mafanikio ..... 20
6.2 Changamoto na Utatuzi ..... 22
7. MWELEKEO ..... 22
8. HITIMISHO ..... 23
9. KIAMBATISHO:Taarifa Hesabu za RUWASA zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ..... 24

## BARUA YA KUWASILISHA TAARIFA

Mheshimiwa Waziri,

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji wa RUWASA kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni 2021. Taarifa hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 53 (1) cha Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 ikilenga kubainisha shughuli zilizotekelezwa na RUWASA katika kipindi cha 2020/2021.

Katika jitihada za kuendelea kuleta mageuzi kwenye utoaji wa huduma endelevu ya maji vijijini, RUWASA inapendekeza kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kusanifu na kujenga miradi ya maji mikubwa inayotumia chanzo kimoja cha uhakika na kuhudumia vijiji vingi badala ya kimoja. Mwelekeo huu, utawezesha kuwa na Vyombo vya Utoaji Huduma katika ngazi ya Jamii (CBWSOs) vichache vyenye wigo mkubwa wa wateja (customer base) utakaoviwezesha kuwa na uwezo wa kimapato ambao ni muhimu katika uendelevu wa huduma ya maji;

(ii) Kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutumia nishati ya jua na kubadilisha mitambo inayotumia dizeli na kuweka umeme wa TANESCO; na

(iii) Kuboresha usimamizi wa mauzo, makusanyo na matumizi ya fedha zinazotokana na mauzo ya huduma ya maji vijijini kwa kufunga dira za malipo kabla ya matumizi (pre-paid meters), kwa kuweka mifumo ya ankara *(unified billing System)* na kujiunga kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG).

Prof. Idrissa Bilali Mshoro
**MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI**

## UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI



Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), ninayo furaha kubwa kuwasilisha Taarifa ya Utendaji wa RUWASA kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021. Taarifa hii, imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 53 (1) cha Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 ikibainisha shughuli zilizotekelezwa na RUWASA katika kipindi cha mwaka 2020/2021.

Taarifa hii ni ya kwanza tangu kuanzishwa kwa RUWASA Julai, 2019. Kutokana na hali halisi kuwa Taasisi ilikuwa ndiyo kwanza imeanza kutekeleza majukumu yake rasmi, wakati wa uanzishwaji wake kulikuwa na haja ya kutekeleza majukumu ya kimkakati yaliyokuwa na lengo lakuweka mazingira wezeshi ya kutekeleza majukumu yake *(operationalization)*, ikiwa ni pamoja na uhamishaji wa mali na madeni *(assets and liabilities)* kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuunda safu ya Uongozi. Uwekaji wa mazingira wezeshi ulihusu pia uhamishaji wa watumishi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zingine za umma. Pia, katika kipindi hicho, uliandaliwa Mpangomkakati wa Muda wa Kati *(Medium Term Strategic Plan)* wa miaka mitano; kutoka 2020/2021 hadi 2024/2025) na usimikaji wa mifumo ya kimenejimenti na kiutawala ili kuhakikisha kuwa RUWASA inatekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya nchi pamoja na kuzingatia kanuni za utawala bora.

Katika kipindi cha mwaka wa 2020/21, RUWASA iliendeleza ujenzi wa miradi ya ujenzi wa skimu za maji vijijini iliyopokelewa kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuibua, kusanifu na kujenga skimu mpya. Aidha, RUWASA ilihuisha vyombo ambavyo awali; kabla ya kupitishwa kwa Sheria tajwa hapo juu, vilijulikana kama COWSOs na kubadili kuwa CBWSOs. Pia, iliunda na kusajili CBWSOs mpya kwa ajili ya uendeshaji wa skimu ambazo ujenzi wake ulikamilika. Uundaji na usajili wa CBWSOs ulienda sambamba na uwezeshaji wa ajira ya watumishi kila CBWSO yenye utaalam wa ufundi na fedha ili kuendana na matakwa ya sheria tajwa. Shughuli hizi na nyingine zilitekeleza kwa kutegemea vyanzo vya Fedha za ndani, ambavyo ni Mfuko wa Maji wa Taifa na Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya nje vilitoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambao ni Benki ya Dunia, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza na UNICEF. Wengine ni Shirika la Misaada ya Kimataifa la Ubelgiji (ENABEL), *UN Habitant* na *Water Mission*.

Ninayo furaha kusema kwamba, licha ya uchanga wake, katika kipindi hicho kifupi tangu kuanzishwa kwake, RUWASA imepata mafanikio ya kujivunia katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini hadi kufikia wastani wa asilimia 72.3, ikilinganishwa na asilimia 64.8 wakati RUWASA ilipoanza

rasmi kutekeleza majukumu yake.. Aidha, RUWASA imeweza kujenga msingi imara wa uboreshaji na uendelevu wa huduma ya maji vijijini. Kasi hii ya kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi waishio vijijini inaleta matumaini ya kufikiwa kwa lengo lililowekwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 la kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa huduma ya uhakika ya maji kwa wananchi waishio vijijini unafikia kiasi kisichopungua asilimia 85.

Nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb) na uongozi wa Wizara ya Maji kwa ujumla kwa maelekezo na miongozo waliyoipatia Bodi na Menejimenti ya RUWASA katika kipindi hicho iliyowezesha kufikiwa kwa mafanikio hayo. Kidhati ninawashukuru Menejimenti na Watumishi wa RUWASA ambao licha ya changamoto zilizopo wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Bodi. Aidha, ninawashukuru Washirika wa Maendeleo niliowataja hapo juu na wengine wengi yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha kwa namna moja au nyingine na utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini. Ushiriki wao katika Sekta ya maji umekuwa na unaendelea kutoa mchango muhimu katika kufikia lengo la Serikali.

Prof. Idrissa Bilali Mshoro

**MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI**

## UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU



Taarifa hii ya Utendaji wa RUWASA ni ya kipindi cha mwaka 2020/2021. Katika kipindi hicho, RUWASA ilitekeleza shughuli mbalimbali zilizojikita katika kutimiza malengo yaliyobainishwa kwenye Mpangomkakati wa miaka mitano; unaonzia mwaka 2020/2021 na kuishia 2024/2025. Malengo hayo, ni Uanzishwaji na Uimarishaji wa Taasisi, Uboreshaji wa Huduma ya Usafi wa Mazingira Vijijini, Uboreshaji wa Utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini, Uboreshaji wa Utendaji wa Rasilimaliwatu, Uwekaji na Uboreshaji wa Mifumo Wezeshi ya Kimejimenti, Umairishaji wa Uwezo na Usimamizi wa Kifedha, Kujenga Taswira ya Taasisi, Uimarishaji wa Mapambano dhidi Maambukizi Mapya ya Virusi vya UKIMWI na Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa.

Jukumu kubwa la RUWASA katika kipindi hicho lilikuwa ni kuendeleza ujenzi wa miradi 632, kati ya miradi 1,847 iliyorithiwa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kukwamua jumla ya miradi 177 iliyokuwa imekamilika lakini haikuwa ikitoa huduma ya maji kwa wananchi kutokana na sababu mbalimbali mojawapo ikiwa ni kukauka kwa vyanzo vya maji. Pia, katika kipindi hicho, RUWASA ilikuwa na jukumu la kuibua miradi mipya kupitia Programu kubwa za zinazofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo, ambao ni DFID na Benki ya Dunia, ambazo ni PbR na PfR, sawia. Aidha, RUWASA ilikuwa na jukumu la kuunda na kusajili Vyombo vya Utoaji wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii *(Community Based Water Supply Organizations – CBWSOs)* ili kuendesha kila mradi mpya uliokamilika na kuhuisha vyombo 3,236 vilivyokuwepo kabla ya RUWASA vya utoaji wa huduma ya maji vijijini, yaani COWSOs na kuvipa hadhi mpya inayoendana na matakwa ya Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019.

Licha ya jukumu zito la usimikaji wa taasisi mpya lililojumuisha uwekaji wa mifumo wezeshi ya kimenejimenti na kiutawala, na changamoto mbalimbali tulizokabaliana nazo kutokana na uchanga wa taasisi, ninayo furaha kubainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho. Miongoni mwa mafanikio hayo, ni ongezeko la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wanaoishi vijijini kutoka asilimia 64.8 iliyokuwepo hadi tarehe 1 Julai 2019 wakati ikianza utekelezaji wake hadi asilimia 72.3 kufikia mwezi Desemba 2020. Ongezeko hili la upatikanaji wa huduma ya maji limetokana na ukamilishai wa miradi 566 kati ya 632 iliyotajwa hapo juu, uibuaji wa miradi mipya 912, ambapo kati ya hiyo, miradi 458 ilikamilika na kutoa huduma kwa wananchi na ukwamuaji wa miradi 115 kati ya 177 iliyokuwa imekamilika lakini haitoi huduma ya maji kwa wananchi. Kwa upande wa uendelevu wa huduma ya maji vijijini, jumla ya Vyombo 2,002 vya Utoaji wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii vilihuishwa na kuundwa.

Mafanikio haya yametokana na uwezeshaji wa fedha za maendeleo zilizotolewa na Serikali kutoka vyanzo vya ndani na nje, ambapo jumla ya Shilingi 494,448,899,837, sawa na asilimia 94 ya bajeti ya fedha za maendeleo iliyoidhinishwa zilitolewa.

Kwa miaka inayofuata, RUWASA itaendelea kujenga skimu za maji kutoka katika vyanzo vya maji vya uhakika na kuimarisha upatikanaji wa huduma endelevu ya maji kwa kujenga uwezo wa CBWSOs. Aidha, suala la usafi wa mazingira litapewa kipaumbele hasa ukizingatia kuwa vijiji vinabadilika na kuwa miji midogo.

Eng. Clement KIVEGALO
**MKURUGENZI MKUU**

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CBWSOs | Community Based Water Supply Organizations |
| COWSOs | Community Owned Water Supply Organizations |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| LGAs | Local Government Authorities |
| OR | Ofisi ya Rais |
| SDG | Sustainable Development Goals |
| DDCA | Drilling and Dam Construction Agency |
| RUWASA | Rural Water Supply and Sanitation Agency |
| REA | Rural Energy Agency |
| TDV | Tanzania Development Vision |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| CRB | Contractors' Registration Board |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| DIT | Dar es Salaam Institute of Technology |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology |
| ERB | Engineers Registration Board |
| DFID | The Department for International Development |
| FCDO | Foreign, Commonwealth & Development Office |
| UNICEF | United Nations Children's Fund |
| GIZ | German Agency for International Cooperation |
| UN-HABITAT | The United Nations Human Settlements Programme |
| ENABEL | Belgian Development Agency |
| RSDMS | Service Delivery Management System |
| PfR | Payment for Results |
| PbR | Payment by Results |

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Uanzishwaji wa RUWASA

Katika kuboresha utoaji wa huduma ya maji vijijini, Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(Rural Water Supply and Sanitation Agency - RUWASA)*. Lengo kuu la kuanzishwa kwa RUWASA ni kuongeza ufanisi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa.

Majukumu ya RUWASA yamebainishwa katika Kifungu cha 43 cha Sheria tajwa hapo juu, ambayo kwa ujumla, ni uendelezaji wa miundombinu kwa kujenga na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji na utoaji wa huduma endelevu ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Kwa mujibu wa Kifungu cha 41 cha Sheria tajwa, RUWASA pia imepewa jukumu la kudhibiti utoaji wa huduma ya maji vijijini kwa kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa Vyombo vya Utoaji wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ambapo kupitia Sheria hiyo tajwa, vyombo hivyo vimepewa jukumu la kuendesha skimu za maji na kuwahudumia wananchi moja kwa moja. Kabla ya kuanzishwa kwa RUWASA, majukumu hayo yalikuwa yakitekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya usimamizi wa kisera wa Wizara ya Maji na uratibu wa OR–TAMISEMI kupitia Sekretariet za Mikoa.

Vilevile, kwa mamlaka aliyonayo kisheria, Waziri wa Maji aliipatia RUWASA jukumu la ziada la kusimamia huduma za maji na usafi wa mazingira katika baadhi ya miji midogo na Makao Makuu ya Wilaya, ambayo kwa ujumla ipo 63. Kati ya hiyo, miji 24 ina Mamlaka za Maji zilizoundwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na Miji 39 bado haijaundiwa Mamlaka za Maji.

## 1.2 Dira, Dhima, Tunu

Katika kutekeleza majukumu yake, RUWASA inaongozwa na Dira, Dhima na kuzingatia Tunu zifuatazo: -

### Dira

Kuwa na Jamii ya wananchi waishio vijijini inayopata huduma ya maji safi na salama, ya kutosha na ya uhakika pamoja na huduma ya usafi wa mazingira.

### Dhima

Kutoa huduma ya majisafi na salama na kuhamasisha usafi wa mazingira kwa jamii iishio vijijini kwa kufanya wa uhakika usanifu, ujenzi, kusaidia uendeshaji na matengenezo ya miundombinu na utoaji wa huduma kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi waishio vijijini.

### Tunu

- Utu;
- Uadilifu;
- Ubunifu;
- Huduma bora;
- Ushirikiano; na
- Utaalam na weledi.

## 1.3 Muundo wa Utendaji na Utawala

Muundo wa uendeshaji wa RUWASA unahusisha ngazi zifuatazo: -

### 1.3.1 Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA

RUWASA ina Bodi ya Wakurugenzi iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019. Bodi hiyo ni tendaji ikiwa na jukumu la kusimamia utendaji wa RUWASA katika utoaji wa huduma ya maji vijijini na kumshauri Waziri mwenye dhamana na maji katika masuala hususan ya kisera yanayohusiana na utoaji wa huduma ya maji vijijini. Bodi hiyo inajumuisha jumla ya wajumbe 9 ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu, ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu na Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za kila siku za RUWASA.

Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wengine wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana na Sekta ya Maji. Wajumbe wa Bodi hiyo wanawakilisha makundi makuu ya wadau, ambayo ni OR–TAMISEMI, REA, CRB, Bodi za Maji za Mabonde, Sekta binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu na Wizara ya Maji.

### 1.3.2 Menejimenti ya RUWASA

Menejimenti ya RUWASA inaundwa na Mkurugenzi Mkuu, Wakuu wa Idara Nne (4) na Wakuu wa Vitengo Nane (8). Idara na Vitengo hivyo ni kama ifuatavyo: -

(i) Idara ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira;
(ii) Idara ya Huduma za Kiufundi;
(iii) Idara ya Mipango na Uratibu wa CBWSOs;
(iv) Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu;
(v) Kitengo cha Ununuzi;
(vi) Kitengo cha Udhibiti wa Ubora;
(vii) Kitengo cha Usimamizi wa Mazingira;
(viii) Kitengo cha Fedha na Uhasibu;
(ix) Kitengo cha Mahusiano ya Jamii na Masoko;

(x) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(xi) Kitengo cha Taarifa na Mawasiliano ya Kiteknolojia na Takwimu; na

(xii) Kitengo cha Huduma za Sheria.

RUWASA inafanya kazi kwenye mikoa 25 isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao unahudumiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam *(Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority – DAWASA).* Katika ngazi ya Wilaya, RUWASA ina ofisi 128. Ofisi hizo zinaongozwa na Mameneja wa Mikoa na Wilaya.

### 1.3.3 Mahusiano na Taasisi Zingine

Katika kutekeleza majukumu yake, RUWASA inashirikiana na taasisi mbalimbali za umma ambazo ni Ofisi za Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Bodi za Maji za Mabonde na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini.

# BODI YA RUWASA



**Prof. Idrissa B. Mshoro**

*Mwenyekiti wa Bodi*



**Sq. Salehe Njaa**

*Mjumbe wa Bodi*



**Eng. Ngwisa Mpembe**

*Mjumbe wa Bodi*



**Prof. Everine Mbede**

*Mjumbe wa Bodi*



**Dkt. Christopher Nditi**

*Mjumbe wa Bodi*



**Eng. Grace Chitanda**

*Mjumbe wa Bodi*



**Eng. Emmanuel Nyanda**

*Mjumbe wa Bodi*



**Eng. Clement Kivegalo**

*Katibu wa Bodi*

## 2. VYANZO VYA FEDHA VYA RUWASA

Katika kipindi husika, RUWASA ilitekeleza majukumu yake kwa kutumia vyanzo vikuu viwili vya fedha ambavyo ni vyanzo vya ndani na vyanzo vya nje, kama ilivyoelezwa hapo chini.

### 2.1 Vyanzo Vya Ndani

(i) Mfuko Mkuu wa Serikali Kuu;

(ii) Mfuko wa Taifa wa Maji (NWIF) ambapo RUWASA inapata mgawo usiopungua asilimia 60 kila mwezi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini; na

(iii) Mapato yanayotokana na uchimbaji wa visima kupitia Sehemu ya Uchimbaji.

### 2.2 Vyanzo Vya Nje

(i) Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID/FCDO) kupitia Mpango wa Malipo kwa Matokeo *(Payment by Results - PbR)*;

(ii) Benki ya Dunia kupitia Programu Endelevu ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira;

(iii) Wadau wengine wa maendeleo ikiwa ni pamoja na UNICEF.

## 3. MALENGO NA MIPANGO

RUWASA inatekeleza majukumu yake ili kukidhi malengo ya kitaifa na kimataifa, ikiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2016 - 2030); Agenda ya Afrika 2063, Awamu ya Tatu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 pamoja na ahadi mbalimbali za viongozi wa kitaifa. Lengo la kitaifa katika kipindi husika ni kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini hadi kufikia kiasi kisichopungua asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Ili kufikia lengo lililoelezwa hapo juu, RUWASA iliandaa Mpangomkakati wa Miaka Mitano *(Medium Term Strategic Plan for 2020/2021 - 2024/2025)* wenye malengo makuu tisa (9) ya kimkakati *(Strategic Objectives)* yafuatayo: -

(i) Uanzishwaji na Uimarishaji wa RUWASA;

(ii) Uboreshaji wa Huduma ya Usafi wa Mazingira Vijijini;

(iii) Uboreshaji wa Utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini;

(iv) Uboreshaji wa Utendaji wa Rasilimaliwatu;

(v) Uwekaji na Uboreshaji wa Mifumo Wezeshi ya Kimejimenti;

(vi) Umairishaji wa Uwezo na Usimamizi wa Kifedha;

(vii) Kujenga Taswira ya Taasisi;

(viii) Uimarishaji Mapambano Dhidi Maambukizi ya Mapya ya Virusi vya UKIMWI; na

(ix) Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa.

## 4. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA RUWASA KATIKA MWAKA 2019/2020

RUWASA ilianza utekelezaji wa majukumu yake rasmi tarehe 1 Jula 2019 ambapo katika kipindi cha 2019/20 jukumu kubwa lilikuwa ni kuisimika taasisi kwa kuweka mazingira wezeshi ya kutekeleza majukumu yake *(operationalization)*, ikiwa ni pamoja na uhamishaji wa mali na madeni *(assets and liabilities)* kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ndizo zilikuwa zikisimamia majukumu ya utoaji wa huduma ya maji vijijini hapo awali. Uwekaji wa mazingira wezeshi ulihusu pia uundaji wa safu ya Uongozi na uhamishaji wa watumishi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zingine za umma. Pia, katika kipindi hicho, uliandaliwa Mpangomkakati wa Muda wa Kati *(Medium Term Strategic Plan)* wa miaka mitano; kutoka 2020/2021 hadi 2024/2025) na usimikaji wa mifumo ya kimenejimenti na kiutawala ili kuhakikisha kuwa RUWASA inatekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya nchi pamoja na kuzingatia kanuni za utawala bora.

Wakati wa Uanzishwaji wake, mwezi Julai 2019, RUWASA ilipokea jumla ya miradi 632 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa iliyokuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. RUWASA pia ilirithi miradi 177 ambayo utekelezaji wake ulikuwa umekamilika lakini ilikuwa haitoi huduma ya maji (Miradi kichefuchefu).

## 4.1 Bajeti ya Kufanikisha Mipango kwa 2019/2020

Katika kipindi cha Mwaka 2019/20, RUWASA ilipanga kutumia jumla ya Shilingi 184,864,406,229 kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 1.

**Kielelezo Na. 1:** *Fedha Zilizopangwa Kutumika Mwaka 2019/2020*




## 4.2 HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO

### 4.2.1 Fedha Zilizopokelewa Kwa Mwaka 2019/2020

Katika kipindi hicho, RUWASA ilipokea jumla ya Shilingi 179,860,845,854, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 97.3 ya bajeti ya fedha za maendeleo iliyoidhinishwa (Jedwali Na. 1). Mchanganuo wa kiasi hicho kwa kila chanzo cha fedha umeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 2.

**Kielelezo Na. 2:** *Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa 2019/2020*



### 4.2.2 Kazi Zilizotekelezwa Kwa Mwaka 2019/2020

#### *(a) Utayarishaji wa Miundokazi na Miongozo*

RUWASA ilifanikiwa kuandaa miongozo 16 inayotumika katika utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo ya utekelezaji wa miradi, uendeshaji wa skimu za maji na utoaji wa huduma, rasilimaliwatu, mipango, na usimamizi wa fedha. Miongozo hiyo ni kama ifuatavyo: -

(i) Mwongozo wa Uendeshaji wa RUWASA;

(ii) Mwongozo wa Usimamizi wa Rasilimalifedha;

(iii) Mwongozo wa Manunuzi;

(iv) Mwongozo wa Upangaji wa Bei za Maji Vijijini;

(v) Mwongozo wa Ujenzi wa Miradi kwa kutumia Watumishi wa Ndani;

(vi) Mwongozo wa Viwango vya Uidhinishaji wa Miradi katika ngazi Mbalimbali;

(vii) Mwongozo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu;

(viii) Mwongozo wa Uendeshaji na Utunzaji wa Miradi ya Maji;

(ix) Mwongozo wa Uundaji na Usajili wa CBWSOs;

(x) Mwongozo wa Mgawanyo wa CBWSOs katika Makundi Mbalimbali;

(xi) Mwongozo wa Uunganishaji wa Maeneo ya Uendeshaji chini ya CBWSOs;

(xii) Mwongozo wa Utumiaji wa Sekta Binafsi katika Uendeshaji wa Miradi ya Maji Vijijiji;

(xiii) Mwongozo wa Uaandaji wa Miradi ya Maji Vijijini;

(xiv) Mwongozo wa Usimamizi wa Mikataba;

(xv) Mwongozo wa Uzingatiaji wa Sheria za Nchi; na

(xvi) Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani.

#### *(b) Uhamishaji wa Mali na Madeni*

Baada ya kuanzishwa kwa RUWASA kulikuwa na uhitaji wa kuhamisha mali na madeni kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mali zenye thamani ya Shilingi Bilioni 759 na fedha kiasi cha Shilingi 29,367,917,204.66 ilitakiwa kuhamishimiwa RUWASA. Katika kipindi husika, RUWASA ilifanikiwa kuhamisha mali kutoka Mamlaka 181 za Serikali za Mitaa na Sekretriet 25 za Mikoa zenye thamani ya Shilingi 608,103,972,981, ikiwa ni takriban asilimia 80 ya lengo. Hata hivyo, kuna Mamlaka za Serikali za Mitaa 5 za Chato DC, Geita DC, Korogwe DC, Bunda DC na Kigoma DC hazikukamilisha kukabidhi mali na fedha. Kuhusu uhamishaji wa fedha, kiasi cha Shilingi 20,480,956,021.94 kilihamishwa. Kiasi kilichobaki yaani Shilingi 8,886,961,182.72 hakikuhamishwa katika kipindi husika kutoka Mamlaka za Serikali mbalimbali.

### *(c) Ujenzi wa Skimu za Maji*

Hadi kufikia Juni 2020, jumla miradi ya 566 ambayo ni sawa na asilimia 89.6 iliyopokelewa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikamilika. Vilevile, katika kipindi hicho, Miradi 115 sawa na asilimia 65 ya miradi 177 ambayo utekelezaji wake ulikuwa umekamilika lakini ilikuwa haitoi huduma ilikamilika



*Mafundi wa RUWASA wakilaza bomba la mradi wa maji wa Mayoka – Minjingu katika Ziwa Manyara utakaohudumia vijiji vya Olasiti, Minjingu, Kakoi na Vilima Vitatu katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara*

## 5. SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2020/2021

Katika kipindi cha Mwaka 2020/21, RUWASA ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 2,610 katika maeneo ya utafutaji wa vyanzo vya maji chini ya ardhi, ujenzi wa mabwawa, usanifu wa miradi na ujenzi wa skimu za maji katika maeneo ya vijijini. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 1 hapo chini.

**Jedwali Na. 1**: *Miradi Iliyopangwa Kutekelezwa Kwa Mwaka 2020/2021*

| Na | Maelezo | Jumla |
|---|---|---|
| 1 | **Utafutaji wa Vyanzo vya Maji** | |
| | 1.1 Uchimbaji wa visima | 542 |
| | 1.2 Ujenzi wa mabwawa<br>• Yanayoendelea (4)<br>• Mapya (8)<br>• Ukarabati (4)<br>• Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina (19) | 35 |
| 2 | **Usanifu wa skimu za maji** | 390 |
| 3 | **Ujenzi wa skimu za maji** | 1,643 |
| | **Jumla** | **2,610** |

Aidha, mbali ya shughuli zingine za usimikaji wa taasisi, za kiutawala, kifedha na uendeshaji wa ofisi, RUWASA ilikuwa na jukumu la kuendelea kuhuisha vyombo (COWSOs) vilivyokuwepo kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 na kukamilisha kazi hiyo kabla au mwishoni mwa mwezi Novemba 2021.

## 5.1 Bajeti ya Kufanikisha Mipango

Ili kufikia lengo kuu la upatikanaji wa huduma ya maji kwa kiasi kisichopungua asilimia 85 ifikapo 2025, RUWASA ilipanga kutumia jumla ya Shilingi 339,760,185,623 katika mwaka wa fedha 2020/21 kamailivyooneshwa kwenye Kielelezo. Na. 3.

**Kielelezo Na. 3:** *Fedha Zilizopangwa kutumika katika mwaka 2020/2021 kutoka Vyanzo Mbalimbali*




## 5.2 Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mipango

### 5.2.1 Fedha Zilizopokelewa

Katika kipindi hicho, RUWASA ilipokea jumla ya Shililingi 345,446,186,212, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 102 ya bajeti ya fedha iliyopangwa kutumika. Mchanganuo wa kiasi hicho kwa kila chanzo cha fedha umeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 2

**Kelelezo Na. 4:** *Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa 2020/2021*



### 5.2.2 Kazi Zilizotekelezwa

#### 5.2.2.1 Uboreshaji wa Utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini

Katika kuboresha utoaji wa huduma ya maji vijijini, RUWASA ilitekeleza kazi mbalimbali zilizogawanywa katika makundi matatu, ambayo ni utafutaji wa vyanzo vya maji chini na juu ya ardhi, usanifu wa miradi mipya na shughuli za ujenzi wa skimu za maji. Kwa upande wa ujenzi, kulikuwa na miradi ya ukarabati na upanuzi wa skimu za zamani na ujenzi wa skimu mpya.

***A: Utafutaji wa Vyanzo vya Maji***

Jumla ya maeneo 230 yalifanyiwa utafiti wa kubainisha yenye uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi. Aidha, visima vipya 212 vilichimbwa na visima 57 vya zamani vilikarabatiwa. Mabwawa mapya 5 yalijengwa. Mchanganuo wa kazi zilizofanyika katika eneo hili la utafutaji wa vyanzo vya maji umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** *Kazi za Utafutaji na Uendelezaji wa Vyanzo vya Maji*

| Na | Shughuli | Mpango | Hatua ya Utekelezji | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % |
| 1 | Utafiti wa maji chini ya ardhi | 400 | 230 | 57.50% |
| 2 | Uchimbaji wa visima | 542 | 212 | 45.00% |
| 3 | Ukarabati wa visima | 50 | 57 | 114.00% |
| 4 | **Ujenzi wa Mabwawa** | | | |
| | (i) Upembuzi yakinifu na usanifu | 19 | 20 | 105.00% |
| | (ii) Ujenzi mabwawa Mapya | 8 | 5 | 62.50% |
| | (iii) Mabwawa yaliyokuwa yanaendelea kujengwa | 4 | 2 | 50.00% |
| | (iv) Ukarabati wa mabwawa | 4 | 1 | 25.00% |



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi RUWASA Prof. Idrissa B. Mshoro mwenye shati jeupe akipewa maelezo na Meneja wa RUWASA Wilaya Mafia alipotembelea uchimbaji wa visima Wilayani hapo.*

### *B: Usanifu wa Miradi*

Jumla ya miradi 482 ilisanifiwa kwa ajili ya ujenzi wa skimu za maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwa na benki ya miradi *(project databank)* yenye miradi itakayokuwa ikitekelezwa kwa miaka inayofuata.

### *C: Ujenzi wa Skimu za Maji*

Jumla ya miradi mipya 912 illibuliwa na kuanza kujengwa, ambapo hadi mwishoni mwa kipindi hicho, miradi 458 (50.2%) ilikuwa imekamilika na kuanza kuhudumia wananchi.

Kukamilika kwa miradi hiyo kuliwezesha jumla vijiji 8,708 kupata huduma ya maji na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 64.8 mwaka 2019 hadi kufikia wastani wa asilimia 72.3 kufikia mwezi Juni 2021.



*Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakishuhudia utiaji wa saini katika mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji vijijini kati ya Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Eng. Clement KIVEGALO pamoja na mmojawapo wa Wakandarasi wa Ujenzi wa miradi ya maji.*




*Mojawapo la Tangi la Maji katika mradi uliojengwa kupitia fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji.*

### 5.2.2.2 Utoaji wa Huduma Endelevu ya Maji

Katika eneo hili la uimarishaji wa huduma endelevu ya maji vijijini, RUWASA ilijikita kuweka misingi ya uendelevu wa huduma, ambapo kazi kuu iliyofanyika ni kuunda na kusajili CBWSOs na kufanya mafunzo ya awali ya kuzijengea uwezo.

#### *A: Uundaji na Usajili wa CBWSOs*

Hadi kufikia mwezi Juni 2021, RUWASA ilikuwa imefanikiwa kuunda, kuhuisha na kusajili jumla ya Vyombo vya Watoa Huduma Ngazi ya Jamii (CBWSOs) 2,450 kati ya COWSO 3,236 zilizopangwa kuhuishwa na kuundwa ifikapo Novemba, 2021.

#### *B: Kujenga Uwezo wa CBWSOs*

CBWSOs zote zilizoanzishwa na kuhuishwa ziliwezeshwa kuajiri jumla ya watumishi 1,746, ambapo kati yao, 940 ni Mafundi na 806 ni Wahasibu. Wajumbe wa CBWSOs na Watumishi wao walipatiwa mafunzo ya awali ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, Mwongozo wa Utoaji wa Mafunzo na Mpango wa Mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo *(CBWSOs' Training Programme)* viliandaliwa.

### 5.2.2.3 Uanzishwaji na Uimarishaji wa RUWASA

Katika eneo la uanzishwaji na uimarishaji wa RUWASA, kazi zilizotekelezwa zimebainishwa hapo chini.

**(i) Uhamishaji wa Mali na Madeni**

Baada ya kuanzishwa kwa RUWASA kulikuwa na uhitaji wa kuhamisha mali na madeni kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mali zenye thamani ya Shilingi Bilioni 759 na fedha kiasi cha Shilingi 29,367,917,204.66 ilitakiwa kuhamishimiwa RUWASA. Katika kipindi husika, RUWASA ilifanikiwa kuhamisha mali kutoka Mamlaka 181 za Serikali za Mitaa na Sekretriet 25 za Mikoa zenye thamani ya Shilingi 608,103,972,981, ikiwa ni takriban asilimia 80 ya lengo. Hata hivyo, kuna Mamlaka za Serikali za Mitaa 5 za Chato DC, Geita DC, Korogwe DC, Bunda DC na Kigoma DC hazikukamilisha kukabidhi mali na fedha. Kuhusu uhamishaji wa fedha, kiasi cha Shilingi 20,480,956,021.94 kilihamishwa. Kiasi kilichobaki yaani Shilingi 8,886,961,182.72 hakikuhamishwa katika kipindi husika kutoka Mamlaka za Serikali mbalimbali.

(ii) **Muundo wa Maendeleo ya Utumishi na Muundo wa Mishahara ya RUWASA**

Kwa mujibu wa miongozo ya kiutumishi, ili Taasisi iweze kusimamia rasilimaliwatu kwa ufanisi inatakiwa iandae Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa RUWASA *(Scheme of Service)*, Muundo wa Mishahara *(Salary Structure)* na kupata Namba ya Fungu *(TR/Vote Number)*. Katika kipindi husika, RUWASA iliandaa Muundo wa Maendeleo ya Utumishi na Muundo wa Mishahara na kufanikisha kuidhinishwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kupatikana kwa Namba ya TR, katika kipindi chote husika, watumishi wa RUWASA walilipwa mishahara kupitia katika Taasisi walizokuwa wakifanya kazi awali kabla ya kuhamia RUWASA.

### 5.2.2.4 Uboreshaji wa Huduma ya Usafi wa Mazingira Vijijini

Katika utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira, RUWASA inashirikiana na Wizara ya Maji; Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto; Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, OR–TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Katika kipindi husika, RUWASA iliendelea na utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na OR-TAMISEMI, ambapo kupitia Programu ya PbR, fedha kiasi cha Sh. 5,334,000,000.00 kutoka DFID kilitumwa kupitia RUWASA na kasha kutumwa kwa wadao hao wanaotekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira katika vituo vya afya na katika shule za msingi na sekondari. Wadau hao pamoja na kiasi cha fedha kilichotumwa ni kama inavyoonekana katika Kelelezo. Na. 5.

**Kielelezo Na. 5:** *Fedha Zilizotumwa Kutekeleza Kampeni ya Usafi wa Mazingira*




Katika kipindi hicho, kiasi cha Sh. 3,602,105,111 sawa na asilimia (68%) ya fedha zilizotolewa kilitumika kuboresha masuala ya usafi wa mazingira katika vituo vya afya, shule za msingi na sekondari ambapo jumla ya vyoo 351 vyenye matundu 1,648 vilijengwa.

### 5.2.2.5 Uboreshaji wa Utendaji wa Rasilimaliwatu

#### (i) Menejimenti ya Rasilimaliwatu

Katika kipindi husika, RUWASA ilikuwa na jumla ya watumishi wapatao 1,670, ikilinganishwa na mahitaji halisi ya watumishi 2,754. Kati ya watumishi hao waliokuwepo, wa jinsia ya kike ni 346 na kiume 1,324. Mchanganuo wa idadi ya watumishi waliokuwepo kwa kila Idara/Kitengo na pengo lake, ni kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 6.

**Kielelezo Na. 6:** *Idadi ya Watumishi wa RUWASA hadi Kufikia Juni 2021*




